


# HALMASHAURI YA MJI KONDOA



MAPENDEKEZO YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2018/2019  
ITAKAYOWASILISHWA KWENYE KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UTAWALA  
TAREHE 15-02-2018.



**HALMASHAURI YA MJI KONDOA**  
**MAPENDEKEZO YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2018/2019**  
**ITAKAYOWASILISHWA KWENYE KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI TAREHE**  
**15-02-2018.**

**1.0 Utangulizi.**

**Mhe. Mwenyekiti**

Halmashauri ya Mji Kondoa ni moja kati ya Halmashauri 8 za Mkoa wa Dodoma. Ilianzishwa mwaka 2015 kutoka wilaya mama ya Kondoa chini ya kifungu namba 8 cha serikali za mitaa kwa sheria namba 7 ya mwaka 1982. Halmashauri ya Mji Kondoa iko umbali wa kilometa 160 kaskazini mwa makao makuu ya Mkoa wa Dodoma. Halmashauri ya Mji Kondoa inapakana na Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa upande wa Kaskazini, Wilaya ya Chemba kwa upande wa Mashariki, Kusini na Magharibi. Halmashauri ya Mji wa Kondoa ina jumla ya tarafa 2, kata 8 na Vijiji 25 na Mitaa 11.

**2.0 Mwelekeo wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019**

**Mhe. Mwenyekiti**

Mwelekeo wa Bajeti 2018/2019 umeandaliwa kwa kuzingatia sehemu kuu tatu (3) nazo ni:-

- I. Mapitio ya Bajeti kwa Mwaka 2016/2017
- II. Mapitio ya Bajeti ya Nusu mwaka (Julai – Disemba, 2017/2018)
- III. Mapendekezo ya Bajeti ya Mwaka 2018/2019

**2.1 MAPITIO YA MPANGO NA BAJETI 2016/2017.**

Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri ya Mji ya Kondoa iliidhinishiwa kukusanya jumla ya **Tsh 15,554,059,741.00** kati ya hizo Halmashauri ilikusanya jumla ya **Tsh 3,523,889,407.00** na kutumia **Tsh 1,400,211,318.00**

**Jedwali Na.1 Mchanganuo wa fedha idhinishwa, Pokelewa na fedhaTumika**

S/n	Maelezo	Kiasi (Tsh)				
		Idhinishwa	Pokelewa	%	Tumika	%
1	Ruzuku ya Matumizi Mengineyo (OC)	1,110,444,000.00	420,956,401.00	38	338,993,254.00	80
2	Ruzuku ya Mishahara	9,317,940,500.00	-	-	-	-
3	Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo	4,296,885,243.00	2,797,580,051.00	65	680,823,871.00	15
4	Mapato ya Ndani	828,789,998.00	726,309,356.00	88	719,387,447.00	99
<b>Jumla</b>		<b>15,554,059,741.00</b>	<b>3,523,889,407.00</b>	<b>23</b>	<b>1,400,211,318.00</b>	<b>39</b>

*Chanzo: Ofisi ya Mkurugenzi Halmashauri ya Mji Disemba 2017*

### 3.0 MAPITIO YA BAJETI KWA NUSU MWAKA 2017/2018

Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Halmashauri ya Mji ya Kondoaliidhinishiwa kukusanya jumla ya **Tsh. 17,202,562,214.00** kati ya hizo Halmashauri ilikusanya jumla ya **Tsh 3,848,467,548.00** na kutumia **Tsh 4,011,320,539.00**

Jedwali Na.2 Mchanganuo wa Mapitio ya Bajeti ya Nusu mwaka 2017/2018

S/n	Maelezo	Kiasi (Tsh)				
		Idhinishwa	Pokelewa	%	Tumika	%
1	Ruzuku ya Matumizi Mengineyo (OC)	503,829,000.00	367,273,000.00	73	359,462,989.00	97
2	Ruzuku ya Mishahara	12,122,498,200	2,045,637,750.00	17	2,045,637,750.00	100
3	Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo	3,450,383,714.00	1,019,111,940	29	1,455,692,081.00	42
4	Mapato ya Ndani	1,125,851,300.00	416,444,858.00	37	150,527,719.00	13
<b>Jumla</b>		<b>17,202,562,214.00</b>	<b>3,848,467,548.00</b>	<b>22</b>	<b>4,011,320,539.00</b>	<b>95</b>

Chanzo: Ofisi ya Mkurugenzi Halmashauri ya Mji Disemba 2017

Miradi ya maendeleo iliyotekelezwa /inayotekelezwa katika mwaka 2017/2018 ni pamoja na

- Ujenzi wa Machinjio Kijiji cha Kingale
- Ujenzi wa Ofisi za Halmashauri ya Mji Kondoali.
- Ujenzi wa Machinjio Kijiji cha Kolo
- Ujenzi wa vyumba viwili na ofisi ya Walimu Shule ya Msingi Damai
- Ukamilishaji wa ujenzi wa ofisi Kijiji cha Unkuku
- Umalizaaji wa nyumba ya Mganga Zahanati Mtaa wa Kichangani.
- Ukamilishaji wa ujenzi wa ofisi ya Kijiji cha Poisi
- Ukamilishaji wa Ujenzi wa Choo cha wanafunzi shule ya Sekondari mto Bubub
- Uchimbaji wa visima na usambazaji wa maji katika vijiji/Mitaa ya Kwapakacha, Maji ya Shamba, Kichangani, Tura, Bolisa, Hachwi na Chandimo.
- Ukarabati na ujenzi wa Vyumba vya madarasa katika shule za Msingi Ubembeni (chumba 1), Mulua (vyumba viwili na ofisi 1), King'ang'a (vyumba viwili na ofisi) na Chang'ombe (vyumba viwili), kupitia fedha za Mfuko wa Jimbo.
- Umalizaaji wa chumba cha maabara Shule ya Sekondari Kwapakacha, umalizaaji wa vyumba viwili na ofisi shule ya Msingi Munguri na Hachwi kupitia fedha za P4R.



**Jedwali Na. 3** mchanganuo wa fedha zilizoidhinishwa Katika mwaka wa fedha 2017/2018,

S/n	Maelezo	Kiasi (Tsh.)
1	Ruzuku ya Matumizi Mengineyo (OC)	503,829,000.00
2	Ruzuku ya Mishahara (PE)	12,122,498,200.00
3	Ruzuku ya Maendeleo (DEV)	3,450,383,714.00
4	Mapato ya Ndani (OS)	1,125,851,300.00
	<b>Jumla Kuu</b>	<b>17,202,562,214.00</b>

*Chanzo: Ofisi ya Mkurugenzi Halmashauri ya Mji Disemba, 2017*

Hadi kufikia Disemba 31, 2017 jumla ya **Tsh 3,848,467,548.00 (21%)** zimepokelewa na **Tsh 4,011,320,539.00 (24%)** zimetumika.

**Jedwali Na. 4** Mchanganuo wa Mapato na Matumizi ya Fedha nusu mwaka 2017/2018

S/n	Maelezo	Mapato	Matumizi	%
1	Ruzuku ya Matumizi Mengineyo (OC)	367,273,000.00	359,462,989.00	98
2	Ruzuku ya Mishahara (PE)	2,045,637,750.00	2,045,637,750.00	100
3	Ruzuku ya Maendeleo (DEV)	1,019,111,940.00	1,455,692,081.00	142
4	Mapato ya Ndani (OS)	416,444,858.00	150,527,719.00	36
	<b>Jumla Kuu</b>	<b>3,848,467,548.00</b>	<b>4,011,320,539.00</b>	<b>105</b>

*Chanzo: Ofisi ya Mkurugenzi Halmashauri ya Mji Disemba, 2017*

### 3.1 Shughuli zilizotekelezwa/zinazoendelea kutekelezwa:-

#### **Mhe. Mwenyekiti**

Miradi yote iliyopata fedha katika mwaka wa fedha 2016/2017, ipo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji. Hali hii imetokana na kuchelewa kwa fedha za maendeleo kutoka serikali kuu



(CDG) na zile za mapato ya ndani. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 fedha za Maendeleo zilizopokelewa ni kama Jedwali linavyoonesha:-

**Jedwali Na. 5 Fedha pokelewa kwa mwaka wa fedha 2017/2018**

S/n	Chanzo	Fedha Idhinishwa	Fedha Pokelewa	Maelezo
1	Serikali Kuu (Ujenzi wa Ofisi za Halmashauri)	1,500,000,000.00	600,000,000.00	Halmashauri inaendelea kusubiri fedha kutoka Serikali kuu.
2	Serikali Kuu (CDCF)	33,090,000.00	16,000,000.00	Halmashauri inaendelea kusubiri fedha kutoka Serikali kuu.
<b>Jumla</b>		<b>1,533,090,000.00</b>	<b>616,000,000.00</b>	

**3.2 Changamoto**

Katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Kawaida na zile za Maendeleo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017, kumekuwa na changamoto zifuatazo:-

- Kuchelewa kutolewa kwa fedha za miradi na zile za matumizi ya kawaida kutoka Serikali kuu
- Ushiriki hafifu wa Wananchi katika shughuli za maendeleo na kuendelea kutegemea Serikali katika kukamilisha miradi yao
- Uwepo wa Migogoro ya ardhi ambayo inazorotesha shughuli za maendeleo
- Upungufu wa watumishi kwa baadhi ya kada kama vile maji, afya, elimu, na ujenzi
- Upungufu mkubwa wa magari.

**3.3. Mikakati**

- Halmashauri imefanya mapitio ya vyanzo vya mapato kwa ushirikiano na LIC (Uboreshaji wa mazingira ya uwekezaji na biashara) ili kufanya maboresho na hatimaye kuongeza mapato ya ndani na kupunguza utegemezi kwa Serikali Kuu
- Kupunguza matumizi katika shughuli za kawaida (recurrent activities) na kuelekeza fedha katika ya shughuli za msingi kwa kipaumbele
- Halmashauri kuendelea kuhamasisha jamii kuongeza jitihada ya kuchangia shughuli za maendeleo katika maeneo yao
- Halmashauri imepanga kufanya utatuzi wa migogoro ya ardhi iliyopo na kuhakikisha migogoro haizaliwi tena na pia kutenga bajeti ya kutosha katika masuala ya ardhi kama kuandaa na kusimamia Mipango ya matumizi bora ya ardhi



- Kupima viwanja katika Kata za Kondoza Mjini, Chemchem na Kilimani na kuviuza ili kuongeza mapato ya Halmashauri.

#### 4.0 MAPENDEKEZO YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2018/2019

Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Halmashauri ya Mji kwa mwaka 2018/2019 yanazingatia mambo muhimu yafuatayo:-

- Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs)
- Dira ya Taifa ya Maendeleo (NDV) 2025
- Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP II) 2016/2017 – 2020/2021
- Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi 2015 – 2020
- Hotuba ya Rais ya Ufunguzi wa Bunge la 11
- Matokeo Makubwa Sasa (Maji, Kilimo, Barabara, Elimu, Mawasiliano, Afya na Biashara)
- Sera mbalimbali za ki-Sekta (Elimu, Afya, Maji, Kilimo na Fedha).
- Miongozo kutoka Serikali Kuu
- Mpango Mkakati na Vipaumbele vya Taifa, Mkoa na Halmashauri.

#### 4.1 UMBILE NA MWELEKEO WA BAJETI MWAKA 2018/2019

Katika mwaka wa fedha 2018/2019, Halmashauri ya Mji Kondoza imepanga kukusanya jumla ya **Tshs 17,202,562,214.00** kwa mchanganuo ufuatao:

Ruzuku ya Matumizi Mengineyo	503,829,000.00
Ruzuku ya Mishahara	12,122,498,200.00
Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo	3,450,383,714.00
Mapato ya Ndani	<u>1,125,851,300.00</u>
<b>Jumla</b>	<b>17,202,562,214.00</b>



## Jedwali Na 6.Mchanganuo wa Ruzuku za Miradi ya Maendeleo

S/n	Jina la Program/Mradi	Makisio (Tsh.)
1	Ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa (LGDG – CDG)	786,069,000.00
2	Mfuko wa Kujenga uwezo(CBG)	87,341,000.00
3	Program ya Maji Vijijini (RWSSP)	61,337,000.00
4	Maombi Maalumu(ujenzi wa ofisi)	1,500,000,000.00
5	Program ya Usafi na Mazingira (RWSSP)	0
6	Mfuko wa Pamoja wa Afya (HSBF)	170,705,000.00
7	Elimu bure (Sekondari)	415,276,000.00
8	Elimu bure (Msingi)	168,249,000.00
9	Kifua Kikuu	6,276,000.00
10	Equip-T	101,679,114.00
11	Mikopo ya Vikundi vya akina Mama	84,111,600.00
12	Program ya Kupambana na UKIMWI (TACAIDS)	0
14	BFFS	12,000,000.00
15	Miradi ya Kilimo DADPS	24,250,000.00
16	Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo (CDCF)	33,090,000.00
17	TASAF III	0
<b>Jumla</b>		<b>3,450,383,714.00</b>

Chanzo: Ofisi ya Mkurugenzi Halmashauri ya Mji Disemba 2017

### 4.2 MAENEO YA KIPAUMBELE.

Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Halmashauri kwa mwaka 2018/2019 yanazingatia kutekeleza maeneo yafuatayo ya kipaumbele katika kukuza uchumi wa ndani:-

#### 4.2.1 Kilimo na Umwagiliaji

- Kuongeza thamani ya mazao mbalimbali mfano Alizeti kwa kuvutia uwekezaji katika eneo la Mongoroma ambapo zimetengwa hekta 3,000 kwaajili ya kilimo cha



umwagiliaji.

- Kujenga stend ya kisasa katika Mtaa wa Bicha ambayo itaongeza mapato ya ndani kutokana na ushuru utakao kuwa unalipwa katika eneo hilo.
- Kuongeza uzalishaji wa zao la mahindi kutoka tani 1.5 hadi 5.75 kwa hekta, alizeti kutoka tani 0.5 hadi 1.7 kwa kutoa mafunzo ya Kilimo bora na kutoa habari za masoko ya mazao kwa **kuanzisha kituo cha Mafunzo, Teknolojia na Habari za Kilimo** na mifugo kilichopo katika Kata ya Chemchem.
- Kupanua biashara ya mazao kwa kujenga/kuanzisha masoko ya mazao katika Vijiji vya **Kolo na Kingale**.
- Kuongeza eneo la shamba la uzalishaji mbegu za kisasa katika eneo la Serya.
- Kushirikiana na sekta binafsi (PPP) katika kutekeleza **kilimo cha mkataba**
- **Kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji:** Halmashauri itaendelea kuwezesha uwekezaji wa ndani kwa kujenga stend (maegesho) ya magari makubwa. Eneo la Bicha (barabara ya Arusha kupitia Babati), kujenga skimu ya umwagiliaji katika Kijiji cha Mongoroma eneo lenye hekta 3,000,
- Kutenga eneo la viwanda lenye ukubwa wa ekari 300 kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vidogo na vya kati.

#### 4.2.2 Mifugo na Uvuvi

Kuongeza ubora na thamani ya mifugo kwa kuongeza uzito wa ng'ombe kutoka kg 150 hadi 250 na mbuzi kutoka kg 20 hadi 30 kwa kufanya yafuatayo:-

- Kuanzisha mradi wa **kunenepesha** mifugo
- Kukarabati josho 1 ambalo halifanyi kazi katika Kijiji cha Serya.
- Kutoa **chanjo** ya magonjwa ya mifugo za CBPP, RVF, FMD, RABIES, LS, BQ na ANTHRAX (Ng'ombe, Mbuzi, Kuku na Mbwa)
- Kuboresha maeneo ya minada (Kolo, Bicha na Iyoli) kwa **kujenga miundombinu** (kujenga uzio kuzunguuka eneo la kuuzia wanyama.
- Ujenzi wa machinjio yanayokidhi vigezo katika Vijiji vya Kolo na Kingale.
- Ujenzi wa Choo eneo la Mnada wa Bicha na Iyoli

#### 4.2.3 Biashara

- Kuwezesha upatikanaji wa huduma na Taarifa za ki Biashara kwa kutumia kituo cha Biashara cha Wilaya
- Kuwezesha mazingira ya kufanya biashara kuwa yenye kuvutia kwa wafanya biashara wadogo na wakubwa.

- Kutoa elimu ya ujasiriamali kwa wafanya biashara wadogo na umuhimu wa kulipa tozo mbalimbali.

#### **4.2.4 Ujenzi**

Katika kuimarisha huduma za miundombinu, Halmashauri imejielekeza katika kuhakikisha kuwa inaboresha mazingira ya kufanyia kazi hasa katika umaliziaji wa:-

- Umaliziaji wa Ofisi ya Mtaa wa Kilimani
- Umaliziaji wa ujenzi wa ofisi ya Mtaa wa Bicha
- Umaliziaji wa ujenzi wa ofisi ya Mtaa Kwapakacha
- Umaliziaji wa ujenzi wa Ofisi ya Kijiji cha Wisi Kwantisi
- Umaliziaji wa chumba kimoja cha darasa shule ya Msingi Kilimani
- Umaliziaji wa Vyumba viwili vya madarasa Shule ya Msingi Iyoli
- Umaliziaji wa Nyumba mmoja ya Mwalimu shule ya Msingi Chemchem
- Umaliziaji wa vyumba viwili vya madarasa Kwamtwaru
- Ukarabati wa vyumba sita vya madarasa Shule ya Sekondari Serya.

#### **4.2.5 Ardhi**

- Kuandaa mpango kabambe wa ardhi na kupima viwanja na kutenga maeneo ya kipaumbele kwa shughuli mbalimbali (Kilimo,viwanda).
- Kutatua migogoro ya ardhi Vijijini kwa kufanya ziara na mikutano na wadau wote wanaohusika kwa kuonyeshana mipaka.
- Kuondoa migogoro baina ya wakulima na gereza la King'ang'a kwa kupanga matumizi bora ya ardhi katika Vijiji vya Chemchem, Iyoli, Kingale na Tampori.

#### **4.2.6 Maliasili na Utalii**

- Kuwezesha ufugaji wa nyuki Kwa kuanzisha mashamba katika msitu wa Kwapakacha, Kingale, na Chemchem.
- Kuhifadhi misitu katika Vijiji vya Kingale, Chemchem, Iyoli na Tampori
- Kuwezesha upandaji miti 1,500,000 katika maeneo yote ya Halmashauri ya Mji.

#### **4.2.7 Elimu Msingi**

Pamoja na kuendelea na utekelezaji wa BRN kwa elimu ya msingi Halmashauri pia itajielekeza katika kutekeleza yafuatayo:-

- Ukamilishaji wa vyumba 3 vya madarasa S/Msingi Munguri
- Ukamilishaji wa nyumba 1 ya mwalimu S/Msingi Chandimo
- ukamilishaji wa vyumba 2 vya madarasa na ofisi moja shule ya Msingi Chandimo
- Ukamilishaji wa darasa moja (1) Shule ya Msingi Ubembeni



- Ukamilishaji wa darasa moja (1) Shule ya Msingi Kilimani
- Ukamilishaji wa choo cha wanafunzi Shule Msingi Gubali
- Ukamilishaji wa matundu nane(8) ya vyoo shule ya Msingi Damai
- Ujenzi wa shule mpya ya msingi kijiji cha serya
- Umaliziaji wa Nyumba ya Mwalimu shule ya Msingi Itiso
- Ujenzi wa choo cha shule ya Msingi Tumbelo
- Ukamilishaji wa nyumba ya Mwalimu (two in one) shule ya Msingi Damai.

#### 4.2.8 Elimu Sekondari

Pamoja na kuendelea kutekeleza vipaumbele, Halmashauri imepanga kufanya yafuatayo:-

- Ukamilishaji wa vyumba tisa (9) vya maabara katika shule za Sekondari za Bicha, Ulla na Dilai. - *Gu yali inestapauliwa*
- Umaliziaji wa Choo shule ya Sekondari Mto Bubu
- Ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Kata Bolisa
- Ukarabati wa vyumba 6 vya madarasa Serya Sekondari. *Maabara*
- Ukamilishaji wa vya

#### 4.2.9 Maji

Katika sekta hii tunapanga kutekeleza yafuatayo:-

- Uchimbaji wa visima kirefu vya Maji katika Vijiji vya Tungufu, Serya na Chemchem
- Usambazaji wa maji katika kijiji cha chadimo, Bolisa, Mulua na Hachwi
- Usambazaji wa maji kutoka kanindo (source) kwenda Mongoroma Kati na Magangaji.
- Ukarabati wa Miundo mbinu ya Maji iliyochakaa katika mitaa ya Chemchem, Iboni, Mnarani, Miningani, Maji ya Shamba na Ubembeni.

#### 4.2.10.0 Afya

- Kupunguza vifo vya akina mama na watoto
- Kuwashirikisha akina baba katika masuala ya uzazi
- Kutoa mafunzo kwa wahudumu wa afya wa jamii (CHWs) juu ya afya ya mama na mtoto.
- Umaliziaji wa nyumba ya Mganga Zahanati ya Kijiji Bolisa.
- Ukarabati mkubwa wa jengo la Zahanati ya Mongoroma.
- Kukamilisha Ujenzi wa nyumba ya mganga katika Zahanati Kichangani
- Kukamilisha ujenzi wa Zahanati kijiji choka
- Kusimamia ukamilishaji wa kituo cha Afya katika Kata ya Kingale.
- Ununuzi wa dawa na Vifaa tiba
- Ukarabati na matengenezo ya vifaa tiba.
- Utoaji wa matone ya Vitamin A kwa watoto.

- Utoaji wa Dawa za mabusha na matende
- Huduma tembezi za mkoba

#### **4.2.10.1 Kuboresha Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF).**

Halmashauri ya Mji Kondoa itaendelea kuboresha Mfuko wa Afya ya Jamii kwa kufanya yafuatayo:-

- Kuongeza wanachama wa CHF kwa kufanya uhamasishaji katika Vijiji 25 na Mitaa 11
- Kuboresha upatikanaji wa huduma kwa wanachama (kwa kuhakikisha upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi)

#### **4.2.10.2 Usafi na Mazingira**

Halmashauri itajielekeza katika kufanya yafuatayo:-

- Kuhamasisha na kusimamia ujenzi wa vyoo bora katika vijiji/Mitaa yote katika Halmashauri ya Mji Kondoa na Taasisi za Umma
- Kutoa elimu ya usafi wa mazingira katika Vijiji na Mitaa yote katika Halmashauri ya Mji Kondoa
- Kuhamasisha wananchi juu ya kuchangia ukusanyaji taka ngumu katika maeneo yao
- Ujenzi wa vyoo eneo la Minada ya Bicha, Kolo na Iyoli
- Ujenzi wa Choo cha stend katika Mtaa wa Ubembeni.
- Ukarabati wa Choo cha Soko kuu Kondoa Mjini.

### **4.3. 0 Masuala Mtambuka**

#### **4.3.1. UKIMWI na magonjwa sugu yasiyoambukiza**

- Kuendelea kuhamasisha watumishi wa Halmashauri kupima afya zao kwa kila robo mwaka kwa ajili ya kupunguza uwezekano wa watumishi kupata magongwa hayo
- Kuendelea kuwasaidia watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi wenye uhitaji katika masuala ya elimu
- Kusaidia vikundi vya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI vinavyojishughulisha na kilimo cha mbogamboga katika Kata zote nane (8) za Halmashauri ya Mji Kondoa.

#### **4.3.2 Mapambano dhidi ya Rushwa**

- Kushirikiana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa katika kubainisha mianya ya Rushwa na kuweka mikakati ya kuzuia rushwa.
- Kushirikiana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa katika kutatua migogoro ya ardhi inayosababishwa na watumishi wasio waadilifu



#### **4.3.3 Uwazi na Uwajibikaji**

- Halmashauri itaendelea kushirikiana na Ofisi ya Maadili ya Utumishi wa Umma katika kuelimisha viongozi wa ngazi zote juu ya masuala ya uwazi na uwajibikaji
- Kusimamia mipango kazi ya wakuu wa idara kuhusu ufuatiliaji wa shughuli zinazotekelezwa katika ngazi za Vijiji na Kata
- Kuendesha mafunzo kwa Viongozi wa Kata, Vijiji na Mitaa yanahusu usimamizi wa fedha zinazoelekezwa katika maeneo yao kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

#### **4.3.4 Lishe**

Halmashauri imepanga kuendelea na utekelezaji wa shughuli za lishe katika sekta za Kilimo, Mifugo, Elimu na Afya kwa kufanya yafuatayo:-

- Kufanya vikao vya kujadili hali ya lishe kwa kila robo mwaka
- Kuendelea kuongeza vikundi vya uhamasishaji lishe kutoka 8 Hadi 16
- Kuendeleza bustani za mbogamboga katika vijiji na Mitaa ya Damai, Wisi kwantisi, Chemchem, Kwapakacha na Unkuku.
- Kuendeleza bustani za mbogamboga na viazi lishe katika shule za Msingi, Sekondari na Zahanati.

### **5.0.KUONGEZA MAPATO YA NDANI NA KUDHIBITI MATUMIZI YA FEDHA**

Ili kuwa na takwimu sahihi za mapato ya ndani, orodha ya walipa kodi, ukusanyaji wa uhakika na kupunguza uwezekano wa upotevu wa fedha, Halmashauri itatekeleza yafuatayo:-

- Kuendelea kutumia mifumo ya kielektroniki katika makusanyo ya fedha (kodi ya majengo, ushuru wa mazao, ushuru wa minada, ushuru wa soko) kwa kushirikiana na Mradi wa LIC (Uboreshaji wa Mazingira ya Biashara na Uwekezaji)
- Kuimarisha mfumo wa kibenki kwa ajili kurahisisha mawasiliano na benki
- Kujenga mazingira mazuri yenye kuvutia biashara katika maeneo mbalimbali ya biashara (minada na masoko)
- Kuwezesha upatikanaji wa gari la mapato
- Kuongeza Watumishi wa Idara ya fedha kwaajili ya kusimamia ukusanyaji wa mapato ya ndani.

Katika kutekeleza vipaumbele hivi, Halmashauri inategemea kukusanya fedha kutoka katika vyanzo vifuatavyo:-

Ruzuku ya Matumizi Mengineyo	503,829,000.00
Ruzuku ya Mishahara	12,122,498,200.00
Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo	3,450,383,714.00
Mapato ya Ndani	<u>1,125,851,300.00</u>
<b>Jumla</b>	<b>17,202,562,214.00</b>

## **6.0. MAOMBI MAALUM**

### **Mhe. Mwenyekiti**

Halmashauri ya Mji Kondo bado ni changa hivyo inakabiliwa na changamoto mbalimbali hasa za miundombinu, hivyo katika Mpango na Bajeti ya Mwaka 2018/2019, inategemea kuomba maombi maalumu kama ifuatavyo.

- i. Ujenzi wa Stendi ya Kisasa Mtaa Bicha **Tsh. 4,500,000,000.00**
- ii. Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika Kijiji cha Mongoroma **Tshs. 600,000,000.00**

**Mhe. Mwenyekiti,**

Kwa heshima na taadhima naomba kuwasilisha,



.....  
(Khalifa Kondo)

**Mkurugenzi Halmashauri ya Mji.  
KONDOA**